HOJA TUNDUIZI

Na. 3

ISBN 978 - 9987 - 710 - 43 - 0

Septemba 2013 • Baraza la Habari Tanzania

KUKUZA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI NA KUHAKIKISHA VIWANGO VYA JUU KABISA VYA WELEDI NA UWAJIBIKAJI

UMUHIMU NA UHALALI WA VYOMBO VYA HABARI KUJISIMAMIA TANZANIA

Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Fredrerick Sumaye akiongea na waandishi wa habari mjini Morogoro mara baada ya kumalizika kwa mafunzo mafupi kwa wahariri wa vyombo vya habari yaliyoandaliwa na MCT.

UMUHIMU NA UHALALI WA VYOMBO VYA HABARI KUJISIMAMIA TANZANIA

Mfanyabiashara maarufu Ali Mufuruki akipeana mkono na Mhariri wa ITV, Stephen Chuwa, baada ya upatanishi uliofanywa na Baraza la Habari Tanzania (MCT). Wanaoangalia ni Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga na Mkurugenzi Mtendaji wa ITV, Joyce Mhaville.

Uhalali wa kujisimamia

TANZANIA ina historia ya miaka 18 ya kuwa na chombo kinachosimamia maadili ya vyombo vya habari. Chombo hiki ni Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Hiki ni chombo ambacho kinapata nguvu na uhalali wake kutoka kwa wanataaluma ya habari na asasi, kampuni na mashirika ambayo vyombo vyake vya habari au kazi zao zina uhusiano wa moja kwa moja – wa mafunzo na utekelezaji, uendelezaji na usimamizi wa maadili ya uandishi wa habari.

Katika mazingira haya, serikali ni mmoja wa wadau. Hii ni kwa kuwa bado inamiliki vyombo vya habari; na linapokuja suala la taaluma na maadili, hakuna kitu kama maadili ya serikali au maadili ya vyombo vya habari binafsi.

Maadili ni yaleyale. Hii pia ndiyo maana wanataaluma kutoka vyombo vya habari vya serikali walishiriki katika kuunda chombo cha usimamizi, kukitumia na kukilinda.

Historia inaonyesha kuwa Baraza lilizaliwa baada ya ukinzani wa muda mrefu (1992–1995); serikali ikitaka kuunda baraza lake na wanataaluma ya habari wakitaka chombo huru, cha hiari na kisichotungiwa sheria.

Hoja na mchango wa mataifa

Kulikuwa na mijadala na kushauriana kwingi kati na baina ya wanataaluma na maofisa wa serikali; ujumbe mwingi kutoka vyama, asasi na mashirika ya habari duniani ukisihi serikali kukubaliana na matakwa ya wanataaluma; na semina ziliandaliwa na tawi la Tanzania la Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika (MISA-Tan) kukazia umuhimu wa kuwepo chombo cha kusimamia maadili ya uandishi kisichokuwa cha serikali.

Hoja za waliotaka baraza la hiari, huru na lisiloanzishwa kwa sheria zilizingatia yafuatayo:

- Shuruti kwa njia ya sheria haijengi nidhamu wala utashi; inajenga woga na woga haujengi.
- Baraza linalotumia mitulinga ya sheria halina ubunifu – linatekeleza lilichoambiwa na serikali.
- Kwa nafasi yake, serikali ndiyo chanzo kikuu cha taarifa. Baraza lake linaweza kutumika kuzuia hata taarifa zilizokuwa zikipenya.

Ujumbe kutoka Tume ya Uhuru wa Habari ya Afrika Kusini ulikuja Tanzania Novemba 2011 kujifunza uzoefu wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) katika mfumo wa vyombo vya habari kujisimamia vyenyewe. Katikati ni kiongozi wa ujumbe huo Mathatha Tsedu ambaye ni Mkurugenzi wa Miradi wa Tume. Wengine ni makamishna wa Tume hiyo Phillip Mtimkulu (kushoto) na Derick Elbrecht (kulia).

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mabaraza ya Habari Duniani (WAPC), uliofanyika katika mbuga za wanyama, Mikumi, 2012. Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) Kajubi Mukajanga ni Rais wa WAPC

Umuhimu na uhalali wa vyombo vya habari kujisimamia Tanzania

- Vyombo vya habari vinaandika juu ya wanasiasa, watawala serikalini – kuwakosoa na hata kukosoa serikali. Kuachia serikali kuunda baraza na kuchunga vyombo vya habari ambavyo ndivyo husimama na wananchi kuichunga serikali, itakuwa ni kuangamiza vyombo hivyo na kuangamiza maoni na sauti ya umma.

- Serikali inatenda mengi yanayohitaji kuchunguzwa. Baraza la kuajiriwa linaweza kudhibiti mtiririko wa habari. Wananchi hawataweza kujua undani wa jinsi serikali inavyowatawala; na serikali haitajua watawaliwa wanataka nini. Hatimaye serikali yaweza kuambiwa tu kile ambacho inataka kusikia.

- Katika mazingira ya aina hii na kwa serikali kuendelea kumiliki vyombo vya habari, na zaidi ya hapo ikawa na baraza, itakuwa moja kwa moja, mgongano wa kimaslahi.

- Mambo mengi ya serikali yanafanywa kwa mtindo wa mazoea; lakini taaluma ya habari inahitaji mawazo mapya kila siku, ubunifu na ushindani; mambo ambayo baraza la serikali haliwezi kusimamia.

- Sheria inayounda baraza yaweza "kuozea" vitabuni na taasisi kudhoofika na kufa (kama SHIHATA), kwa kuwa kinachotekelezwa ni kile tu kilichoko kwenye karatasi.

Dhana ya kujisimamia

Kujisimamia katika uandishi wa habari, ni kufanya kazi ya uandishi, ukiongozwa na maadili yaliyokubaliwa katika taaluma; bila shuruti ya serikali au mamlaka nyingine; na bila sheria za kukazia maadili.

Umuhimu na uhalali wa vyombo vya habari kujisimamia Tanzania

Wanataaluma wanakuwa chini ya chombo chao cha hiari na huru, ambamo msukumo wa uandishi bora unatokana na jukumu la kuwa jicho, sikio na mdomo wa jamii. Humu kuna "mapenzi" ya kazi, utashi, nia ya kufanikisha jukumu na joto la kuwa mshindi – kwa kupakua kilicho bora.

Dhana ya tasnia ya habari kujisimamia yenyewe inatokana na nafasi ya habari katika jamii – kiwezesho cha watu katika jamii husika kupata taarifa, habari na maarifa; kuzitumia kudadisi na kuhoji; kufikiri zaidi na kupembua na kuweza kuwa na maoni na kufanya maamuzi sahihi juu ya kile ambacho kinawagusa au kuwahusu.

Kwa hiyo, kwa watu waliodhamiria kufanya kazi ya uandishi wa habari kwa weledi na uadilifu, kujisimamia kunalenga kuinua na kukuza ubora wa uandishi wa habari; kupunguza uwezekano wa kuingiliwa na serikali; na hivyo, kulinda uhuru wa mwandishi, uhuru wa wananchi kupata habari na uhuru wa vyombo vya habari (kupata, kukusanya na kusambaza habari).

Na kwa kuwa kupitia uhuru huu wananchi wanaweza kuhoji watawala wao na vyombo vya habari vinaweza kusimama na wananchi kuchunga serikali yao (watawala), hakujapatikana chombo cha kulinda ipasavyo uhuru wa jamii ya wanataaluma, weledi na waaminifu kwao na kwa umma, kama tasnia yenyewe kujituma, kujielekeza na kujichunga bila shuruti ya sheria.

Wanataaluma ya habari huwa tunaulizana: Hivi kati ya habari bora na uhuru wa kuandika, kipi kinakuja kwanza? Wengi huwa wanasema sharti uhuru uje kwanza. Ndani ya serikali nyingi huwa wanasema, kwanza kuwepo na uandishi bora ndipo "muwe na haki ya kupata uhuru."

Katika mazingira haya, ukiachia serikali iunde baraza la habari, baraza laweza kuchukua sura na tabia ya watawala kabla ya uhuru. Watawala wa wakati huo walikuwa wakisema, "hamjafikia hatua ya kujitawala."

Kunahitajika kwanza mazingira yanayotoa uhuru wa kuandika; na kama hayapo yapiganiwe na Baraza, mara hii kupitia mfumo wa kujisimamia; ndipo tuanze kutafuta ubora wa kazi ndani ya mazingira huru. Huwezi kupata uandishi bora katika mazingira ya kifungo.

Pamoja na kwamba kuna serikali ambazo zinaweza kuruka kamba na kuingilia Baraza na uhuru wa waandishi; nyingine kushindwa kutumia mifumo yake ya kupata haki (mahakama); na badala yake kufungia vyombo vya habari (Uganda: Gazeti la Monitor na TV yake; Tanzania: MwanaHALISI na mengine); dunia itaona kuwa serikali siyo adilifu.

Mfumo wa kujisimamia

Kunaweza kuwepo njia mbalimbali za kujisimamia lakini njia mbili maarufu ni:

(a) Chombo cha habari chenyewe kuweka utaratibu wa kujichunga kwa kuajiri mtu mwenye taaluma ya habari, mweledi, mwaminifu, ili awe anapitia machapisho au kusikiliza redio na kutazama televisheni, kisha kutoa maoni kwa wahusika ili makosa yasahihishwe na marekebisho yafanywe.

Huyu aweza pia kuwa anapokea maoni ya wadau wa chombo husika – pongezi, malalamiko na shutuma; na baadaye yakatolewa majibu au ufafanuzi. Kwa njia hii waweza kupunguza makosa, kuongeza stadi za waandishi, kuwa karibu na wananchi

Umuhimu na uhalali wa vyombo vya habari kujisimamia Tanzania

walioulizia maswali au waliolalamika; na kwa njia hiyo ukaongeza mauzo, usikilizaji au utazamaji wa chombo chako.

(b) Baraza la Habari. Hii ndiyo njia inayotumika sana na yenye tija zaidi. Tukichukua mfano wa MCT, baraza linaleta pamoja wanataaluma wengi wa viwango mbalimbali na kujenga umoja thabiti.

Linakusanya wamiliki wa vyombo vya habari na asasi mbalimbali zenye mrengo huohuo, kuwa wanachama wa mtandao mpana wa kujisimamia na linasimamia utungaji maadili ya taaluma na taratibu za kuyatekeleza.

Baraza linafuatilia utekelezaji wa maadili katika vyombo vya habari – kwa kutolea maoni utendaji wao kwa njia ya kukosoa, kuelimisha na kuonya; mambo ambayo yanasaidia kujenga imani ya jamii katika uandishi na vyombo vya habari; linaanda mafunzo ya kukuza stadi; na kuunda "Mahakama ya Ridhaa" (Court of Honour) kusikiliza malalamiko ya wadau na kuyatolea uamuzi.

Baraza linakuwa sauti ya waandishi wote hata wale ambao vyombo vyao havijajiunga nalo; linapigania uhuru wa habari, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa wahariri – kwa kutoa miongozo na kwa kushiriki katika juhudi za kuandaa mapendekezo ya kuachana na sheria katili za habari.

Jambo muhimu hapa ni kwamba, kuwepo kwa Baraza, hakuzuii chombo binafsi kujipekua, kujitathmini, kujisahihisha na hivyo kupunguza malalamiko ya wadau wake. Kwa hiyo chombo kinaweza kuchanganya – utaratibu wa binafsi na ule wa pamoja – katika Baraza ambalo lina mtandao na ushawishi mpana wenye sauti na nguvu moja.

Faida za kujisimamia kwa Baraza

Uzoefu umeonyesha kuwa kutumia Baraza la hiari, huru na lisilotungiwa sheria, kuna manufaa mapana.

(a) Kunajenga mazingira huru ya kuwa na mijadala na maafikiano kwa misingi ya kidemokrasia.

(b) Kunalinda, kutetea na kuhalalisha haki ya mwandishi ya kuwa huru.

(c) Kwa kutumia Mahakama ya Ridhaa, kumaliza malalamiko na mashauri mengine yanayohusu waandishi na vyombo vyao, utaratibu ambao unasaidia kupunguza mashauri katika mahakama (mahakama ya sheria).

(d) Walalamikaji wanahudumiwa haraka kwa kuwa hakuna taratibu ndefu za mafaili na hati mbalimbali; maamuzi yanapatikana haraka pale ambapo pande zinazohusika zitafanya haraka kutimiza masharti machache na mepesi wanayopewa – kwa mfano maelezo muhimu ya anacholalamikia au kuonyesha nyaraka ambazo muhusika anatumia kujengea malalamiko yake.

(e) Hakuna gharama za kufungua shauri kama ilivyo katika mahakama za sheria.

(f) Mfumo wa Baraza unalenga kuthibitisha ubora wa kazi ya uandishi ambao unasisitizwa na maadili. Kwa hiyo, hii inakuwa fursa nyingine ya uwezeshaji kitaaluma.

(g) Baada ya maelezo na majadiliano, kuna wanaokuta kumbe wasingelalamika; kwa hiyo wanakuwa wamepata elimu jinsi vyombo vya habari vinavyofanya kazi.

(h) Maamuzi ya Baraza yanaleta faraja na kuridhika kwa pande zote; lakini faraja zaidi pale upande mmoja unapoona mwingine umekubali makosa waziwazi na kwa hiari.

(i) Linapatikana funzo kwa serikali kuwa siyo kila kitu kinakwenda kwa shuruti au shinikizo la sheria.

Katika kujenga mshikamano wa waandishi wa habari na wamiliki wa vyombo vya habari, kupigania mazingira bora ya kufanyia kazi ya uandishi, kuondosha sheria kandamizi na kuwezesha waandishi kupata mbinu, stadi na maarifa zaidi hasa kwa sasa, hakuna kama Baraza la Habari Tanzania.

TAMKO LA TANGA KUHUSU UMUHIMU WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI KUENDELEA KUJISIMAMIA VYENYEWE

Sisi Wahariri kutoka vyombo mbalimbali vya habari, tuliokutana tarehe 29 hadi 30 Mei, 2013 katika Mkutano wa Pili wa Mashauriano kati ya Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri (TEF);

Tukizingatia wajibu wetu wa kusimamia ukusanyaji, utayarishaji na utoaji habari kwa umma;

Tukiamini kuwa vyombo vya habari vina dhima kubwa katika kukuza demokrasia na utawala bora nchini;

Tukijua umuhimu wa wanahabari kuzingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari ili kuupa umma habari sahihi na za kweli na kuwawezesha kufanya maamuzi;

Tukiamini kuwa njia bora ya kuboresha weledi na uzingatiaji maadili ya uandishi wa habari na kuendeleza imani ya umma kwa vyombo vya habari ni kwa kutumia Baraza la hiari na huru ambalo kwa sasa limekomaa katika utendaji kazi wake;

Tukizingatia mafanikio makubwa katika miaka 18 ya waandishi kujisimamia, kujisahihisha, kujielimisha na kujirekebisha chini ya Baraza la Habari la hiari na huru; na matumizi bora ya mahakama yake ya ridhaa;

Tukijua kuwa kuna jitihada mpya sasa za kujaribu kufifisha juhudi za waandishi wa habari na kuwanyang'anya uhuru wao wa kujisimamia chini ya Baraza la Habari kama ilivyojionyesha katika hotuba ya Waziri wa Habari bungeni Mei 20, 2013 na matamko mbalimbali ya wabunge;

Mhariri kutoka Magazeti ya Uhuru na Mzalendo Jane Mihanji akitoa hoja katika Mkutano wa Pili wa mashauriano kati ya Baraza la Habari Tanzania na wahariri wa vyombo vya habari nchini uliofanyika Mei, 2013 mkoani Tanga.

TAMKO LA TANGA KUHUSU UMUHIMU WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI KUENDELEA KUJISIMAMIA VYENYEWE

Tukielewa kuwa kudhibiti waandishi wa habari ni kuwanyang'anya uhuru wa kutenda kazi zao na hivyo kujenga mazingira ambamo umma utaweza kukosa taarifa na habari muhimu kwa manufaa yao;

Kwa hiyo basi:

1. Tunataka ifahamike kwamba wahariri na waandishi tuna imani na Baraza la Habari Tanzania; na kwamba limefanya kazi yake kwa mafanikio makubwa katika kuhakikisha waandishi wanajisimamia, wanajielimisha, wanajisahihisha na kujirekebisha.

2. Tunasisitiza kuwa Baraza limekidhi haja ya kuundwa kwake katika kipindi chote cha miaka 18 ambamo limesikiliza na kutolea maamuzi malalamiko ya wananchi wakiwemo viongozi wa serikali na hata serikali yenyewe.

3. Tunataka ifahamike kuwa tunapinga juhudi zozote za mtu binafsi au kikundi za kujaribu kuingilia kazi za Baraza au kuandaa mazingira ya kulidhoofisha au hata kulifuta.

4. Tumezingatia kwa aina ya kipekee kauli ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mathias Chikawe(MB) ambaye kwa hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano huu, ameahidi serikali kulinda waandishi wa habari na hata kuchunguza mazingira ambamo watakuwa wamekumbwa na majanga.

5. Tunaahidi kuendelea kupigania uhai wa Baraza la Habari na kazi yake bora na tunaahidi kusimama na Baraza na Jukwaa la Wahariri katika kutimiza jukumu letu la kuhudumia umma wa Tanzania.

Waziri wa Katiba na sheria Mh. Mathias Chikawe akijadiliana na Mkurugenzi wa Mfuko wa Waandishi wa Habari (TMF) Bw. Ernest Sungura (kushoto), Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF) Bw. Theophil Makunga (wa pili kulia) na Mshauri wa Habari Bw. Ndimara Tegambwage. Waziri Chikawe alikuwa mgeni rasmi kwenye Mkutano wa Pili wa Mashauriano kati ya wahariri na MCT uliofanyika mkoani Tanga Mei, 2013 (Picha na Paul Mallimbo, MCT)